



Fifth EsF Assembly
Hyderabad, India
30 July-August 13, 2016

Montessori Education for Social Change
Serving Humanity - Celebrating Solidarity

2016 EsF Assembly Daily Summary

Tuesday, 9 August 2016

Lynne Lawrence alifungua kikao cha asubuhi na nukuu toka kwa Mario Montessori. Jennifer Moore toka Afrika ya Kusini alielezea kuwa nchini mwao leo ni Siku ya Wanawake Kitaifa na alitualika kutafakari juu umuhimu wa kazi ya wanawake. Charo Alarcon Mkurugenzi wa shule iliyopo kwenye jumuiya ya Lumin Wesley Rankin aliwasilisha mada yake ya siku iliyohusu Kanuni za Montessori katika jumuiya za kimaskini. Alitushirikisha hadithi kazi iliyokuwa ikifanyika kwenye Shule ya Jumuiya iliyo katika Ziwa Lumin Bachman. Kazi ya shule hii huanzia pale wazazi wanapokuwa wajawazito na wanatoa elimu kwa wazazi kwa ajili ya familia ambazo zina watoto wachanga na wale wanaotambaa. Charo alielezea changamoto na mafanikio ya kazi yake katika jumuiya inayozungumza lugha mbili na jinsi inavyokuwa kwa wakati. Alitoa dondoo kama anza ukiwa kijana na shirikisha wazazi.

Baada ya chai ya asubuhi, washiriki walijigawa katika makundi yao ya kazi kwa ajili ya kazi zaidi za kuendeleza kanuni za WwM. hili liliendelea mpaka baada ya chakula cha mchana mpaka muda ule wazi ambapo mada mbili ziliwasilishwa. Mada ya kwanza kuwasilishwa ilikuwa ya mshiriki wa mkutano wa WwM John Hemanth Kumar Gaddam, ambaye nanafanya kazi kama mwanasaikolijia kwa watoto waliokatika mazingira hatarishi. John alitushirikisha uzoefu wake na kuwakumbusha washiriki umuhimu wa kujitambua wenyewe. Mada ya pili iliwasilishwa na Michael Monteiro ambaye ndiye aliyekuwa mchukuaji picha kwa kundi hili la WwM. Michael alzungumzia uzoefu wake wa kufanya kazi na Divya Disha, Taasisi isiyokuwa yakiserikali ambayo ilianzishwa mwaka 1987, ambayo ilitafuta kuwa wakala wa mabadiliko, kwa kuwawezesha kila mmoja na mashirika katika safari ya kufikia maendeleo ya kiujumla/pamoja. Historia ya Michael ilianza kwenye mitaa ambazo zinajishughulisha na Virusi/Ukimwi, Madawa, Uhalifu, Makazi duni, Ajira kwa watoto, Unyanyasaji wa watoto na mambo mengineyo ambayo yaliwaunganisha washiriki.

Kilichofuata kwenye muda wa wazi wa uwasilishaji ilikuwa kwa washiriki kuhudhuria moja ya warsha zilizohusu Ujana, Teknolojia na Malezi ya watu wenye umri mkubwa (wazee).
